| Martin J. Mmari | Chairman - Non- Executive Director | Mwenyekiti | 1,122,500 |
| Boniface C. Muhegi | Non-Executive Director | Mjumbe | 1,867,794 |
| Bede P. Lyimo | Non- Executive Director | Mjumbe | 200,000 |
| Ally H. Laay | Non- Executive Director | Mjumbe | 160,945 |
| Kai Kristoffersen | Non- Executive Director | Mjumbe | 0 |
| Juma A. Abdulrahman | Non-Executive Director | Mjumbe | 193,650 |
| Hon. Frederick T.Sumaye | Non- Executive Director | Mjumbe | 6,206,980 |
| Ms. Selina A. Mkony | Non –Executive Director | Mjumbe | 32,250 |
| Ms. Rose F. Metta | Non-Executive Director | Mjumbe | 13,514 |
| Mr. Adam H. Mayingu | Non-Executive Director | Mjumbe | 79,200 |
| Dr. Charles S. Kimei | Managing Director, Ex officio | Mkurugenzi Mtendaji | 993,122 |

Uongozi wa Benki

Benki inaongozwa na Mkurugenzi mtendaji akisaidiwa na kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma Shirikishi na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Uendeshaji na

Management Team

Management of the Bank is under the Managing Director assisted by Deputy Managing Director Shared Services and Deputy Managing Director Operations and

Huduma kwa Wateja. Mkurugenzi wa Viashirishi vya hatari, Mkurugenzi wa Mikakati na Uvumbuzi na Mkurugenzi wa Masuala ya Wanahisa wao huripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma Shirikishi anasimamia kurugenzi za Fedha, Utawala, Mawasiliano na Jasiliamari watu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Uendeshaji na Huduma kwa Wateja husimamia kurugenzi za Mikopo, Wateja wadogo, Wateja Wakubwa, Masoko, Utafiti na Huduma kwa Wateja, Huduma Mbadala and Hazina. Idara zote zinaongozwa na wakurugenzi.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji Uendeshaji na Huduma kwa Wateja anasimamia mikopo, huduma kwa wateja binafsi, Huduma kwa wateja wakubwa na kampuni, Masoko, Utafiti na Huduma kwa wateja, Huduma Mbadala za Benki, na Hazina. Idara zote zipo chini ya wakurugenzi.

Mkurugenzi wa Ukaguzi wa ndani anaripoti moja kwa moja kwa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi .

Kamati za Uongozi

Uongozi wa Benki ya CRDB unazo kamati sita ambazo ni;

Kamati ya uongozi wa Juu

Kamati ya Uongozi wa juu inakutana walau kila robo mwaka ili kujadili na kuangalia upya ufanisi wa mikakati ya benki na mpango mkakati. Lengo kubwa la kamati ni kutoa muongozo kwa kampuni na kuhakikisha rasilimali ya benku inatumika kwa ufanisi. Kazi zingine za kamati hii ni pamoja na;

Kutengeneza na kupitia kila mara sera kwa ajili ya kupitishwa na Bodi.

Kuangalia utekelezaji na kusimamia dira ya Benki, mikakati na mpango kazi wa benki.

kuanzisha mikakati ya ujumla ya benki na malengo ya kifedha zitakazokubalika na Bodi, pia na malengo ya mmoja mmoja na ya idara pamoja na malengo ya fedha.

Kusimamia malengo kwa kulinganisha na mipango mikakati ya benki na kuchukua hatua sahihi kuboresha utendaji.

Kuangalia tija katika kila uwekezaji au uanzishwaji wa biashara au kuachia biashara yoyote iliyochini yake au kwa kupitishwa na bodi.

Customer Service. Director of Risk and Compliance, Director of Strategy and Innovations and Director of Corporate Affairs also report directly to the Managing Director.

The Deputy Managing Director Shared Services oversees the Finance, Administration and General Services, Information and Communication Technology and Human Resources departments. All the departments are headed by Directors.

The Deputy Managing Director Operations and Customer Service oversees the Credit, Retail Banking, Corporate Banking, Marketing, Research and Customer Service, Alternative Banking Channels and Treasury departments. All the departments are headed by Directors.

The Director of Internal Audit reports directly to the Board Audit Committee.

Management Committees

The Management of CRDB Bank has six committees as follows:

Executive Committee

The Executive Committee meets at least quarterly to discuss and review the effectiveness of the Bank's strategies and strategic plans. The main objective of the Committee is to provide leadership to the Group and ensure efficient deployment and management of the Bank's resources. Other functions of the Committee include:

- Develop and periodically review policies for Board approval;
- Oversee implementation and monitor the Bank's corporate vision, strategies, and business plans;
- Formulate the Bank's overall strategy and financial targets that are to be agreed with the Board, as well as individual business and functional strategies and financial targets;
- Monitor performance against strategic plan of the Bank and taking appropriate actions to improve performance;
- Review viability of any acquisition or establishment of any new business or disposal of any business within its mandate or for board approval;
- Review and recommend annual budget to the Board for approval.

Management Committee

The Committee is responsible for reviewing and monitoring implementation of operational plans to

Kuangalia na kupendekeza bajeti ya mwaka kwa kupitishwa na bodi.

Kamati za uongozi

kamati zinawajibu wa kupitia na kusimamia utekelezaji wa mipango ya uendeshaji kuhakikisha utambuzi wa changamoto na baadhi ya mambo yanayoweza kuathiri kutofikiwa kwa malengo ili kuyatafutia ufumbuzi. Hukutana kwa mwezi mara moja.

Kamati ya Usimamzi wa Rasilimali na Madeni

Kamati hukutana kila mwezi na inaweza kufanya mkutano wa dharula inapojitokeza dharula inayohitaji maamuzi ya haraka. kamati inamajukumu yafuatayo;

Kusimamia mizania kuhakikisha rasilimali zinawekwa panapostahili kufikia malengo ya utendaji.

Kupitia hali ya ukwasi uliopo na ule unaotarajiwa na kusimamia vyanzo mbadala vya uwekezaji kuhakikisha kuna ukwasi wa kutosha unakuwepo muda wote.

Kupitia viwango vya mtaji kwa sasa na kwa baadae kuangalia utoshelezi kwa ajili ya ukuaji na ubora wa rasilimali.

Kupitia utendaji halisi kwa kulinganisha na malengo/matarajio na bajeti na kuangalia sababu za kutofikia kwa maamuzi ya wakati.

Kupima na kusimamia hatari za uwekezaji kwa benki kwa muendeleo na kuhakikisha hali nzuri ya rasilimali inakuwa katika viwango vilivyowekwa na bodi na sheria za Benki Kuu ya Tanzania.

Kamati ya Mikopo

Kamati inakutana walau maramoja kwa wiki. kamati ina majukumu yafuatayo:

Kupitia na kupendekeza kupitishwa kwa maombi ya mikopo ambazo zipo nje ya kiwango cha Mkurugenzi mtendaji.

Kusimamia na kuangalia upya mikopo inayohitaji kugeuzwa na tarifa za marejesho ya mikopo na kutoa muongozo kwa hatua zinazopaswa kuchukuliwa kuboresha ubora wa mikopo

Kuangalia kwa walau maramoja kwa kila robo mwaka hali ya mikopo, mikopo inayoweza kutolewa kulinganisha na viwango vilivyowekwa na kufuata viwango vilivyowekwa kisheria.

ensure timely identification of challenges and issues that might affect the achievement of targets for remedial action. It meets at least monthly.

Asset Liability Management Committee

The Committee meets at least monthly and may hold extra-ordinary meetings on the occasion of exceptional events requiring immediate decision making. The Committee is responsible for:-

- Managing the balance sheet to ensure proper allocation of resources to achieve performance targets;
- Reviewing the current and prospective liquidity positions and monitoring alternative funding sources to ensure adequate liquidity is maintained at all times;
- Reviewing the current and prospective capital levels (risk based) to determine its adequacy in relation to expected growth and asset quality;
- Reviewing the actual performance against established targets/projections and budgets and analyzing the reasons for any variances for timely actions;
- Measuring and monitoring the investment risk of the Bank on an ongoing basis and ensuring a quality portfolio of assets is maintained within the limits set by the Board and Bank of Tanzania regulations.

Credit Committee

The Committee meets at least once a week. The Committee has the following duties:-

- Review and recommend for approval credit applications that are above the approving authorities of the Deputy Managing Director;
- Monitor and evaluate weekly turnaround and recovery reports and provide guidance on the actions to be taken to maintain quality of loan portfolio;
- Reviews at least quarterly loan portfolio trend, exposure against limits and compliance to BOT, regulations.

Risk Committee

The Management Risk Committee oversees risk management practices in the Bank. The Committee meets monthly under the Chairmanship of the Managing Director and is attended by all Heads of Departments.

The main responsibilities of the Committee are:-

- Implementing strategies and policies of the Board on risk management;

Kamati ya Viashiria vya hatari

Kamati ya udhibiti wa viashiria vya hatari inatazama maeneo ya hatari katika utendaji wa Benki. Kamati inakutana maramoja kwa mwezi chini ya uenyekiti wa Mkurugenzi Mtendaji na inahudhuriwa na Wakuu wote wa Idara.

Majukumu ya kamati hii ni;

Kutekeleza mikakati na sera za Bodi za udhibiti wa hatari.

Kusimamia hatari zinazoweza kujitokeza kupitia viashiria vikuu vya hatari na kuamua juu ya hatua zinazofaa kudhibiti hatari hizo.

Kusimamia mifumo ili kupima, kusimamia na kudhibiti hatari sambamba na utoaji taarifa kwa Bodi na kamati ya udhibiti wa hatari kwa viwango vya hatari hizo na mikakati ya udhibiti wa hatari hizo.

Kamati ya Zabuni

Kamati inahusika katika kuangalia taratibu za manunuzi ya benki kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji. Kazi kuu za kamati ni pamoja na kutambua wazabuni bora, wakandarasi na washauri wataalamu kama inavyohitajika, kuidhinisha kwa taratibu za manunuzi zitakazotumika na kupendekeza ikiwa kuna itakayohitaji kuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji iliyo nje ya taratibu zilizopo ikiwa kutakuwa na haya ya kufanya hivyo.

Mahusiano na Wadau

Katika kutimiza wajibu, wakurugenzi wanaamini wanaongoza kwa mujibu wa maslahi ya wanahisa, wakati huohuo ikizingatia pia maslahi ya wadau wengine katika kampuni ikiwa ni pamoja na wadhibiti, wateja, wafanyakazi na wazabuni. Wakurugenzi watendaji wanamawasiliano ya mara kwa mara na wanahisa wakubwa kwa mwaka mzima, kwa kuhudhuria majadiliano na wawekezaji pamoja na mikutano ya wanahisa. Mrejesho wa mikutano hiyo inapelekwa kwenye Bodi. Benki inaendelea kuboresha mahusiano mazuri na wadau wake wote. Wanahisa wanahimizwa kuhudhuria Mkutano wa wanahisa au kuteua wawakilish wao ikiwa watashindwa kuhudhuria. Tunazo ajenda za Mkutano Mkuu zinazompa fursa mwanahisa kuchangia maoni kwenye majadala katika mkutano huo.

Wanahisa wanahimizwa kuelekeza maswali yao kwenye menejimenti na Bodi na kutoa maoni kwenye tovuti ya Benki. www.crdbbank.com.

- Monitor risk exposures through key risk indicators and deliberate on the actions to mitigate them;
- Implementing systems to measure, monitor and control risk together with regular reporting to the Board and its risk Committee on the level of exposure to various risks and implemented/proposed mitigation strategies.

Tender Committee

The Committee is responsible for oversight of the tender process in the Bank as delegated by the Managing Director. The main duties of the Committee includes identification of competent suppliers, contractors and consultants as required, approval of the procurement methods to be used and recommend or approval by the Managing Director exceptions from the stipulated procurement method in case of an emergency.

Relationship with Stakeholders

In fulfilling their responsibilities, the Directors believe that they govern the Group in the best interests of shareholders, whilst having due regard to the interests of other stakeholders in the Group including regulators, customers, employees and suppliers. The Executive Directors have regular and ongoing communication with major shareholders throughout the year, by participating in investor presentations and shareholders meetings. Feedback from these meetings is reported to the Board. The Bank continues to maintain good relationship with all Stakeholders. Shareholders are encouraged to attend the AGM or appoint proxies to represent them in case they fail to attend. We have a standing agenda in the AGMs which allows the shareholders to contribute their ideas on issues to be discussed during the meetings.

Shareholders are encouraged to direct questions to management and the Board and give comments through the Bank's website: www.crdbbank.com.

There is a dedicated Registrar Office under Corporate Affairs Department to handle shareholders issues immediately as they arise such as payment of dividends, transfer of shares and shareholding matters in general. Investor relations unit is also responsible for providing public information to both existing and prospective investors.

Insider Trading

The Bank has an Insider Trading policy providing guidance on the conduct of insiders in the trading of its shares. Insiders are allowed to trade three days after disclosure of quarterly, annual financial results and any

Yupo ofisa katika kitengo cha Mambo yahasuyo kampuni kwa ajili ya masuala ya wanahisa kama vile malipo ya gawio, kuhamisha hisa na masula yahasuyo hisa kwa ujumla. Kitengo cha mahusiano na Wawekezaji pia kinawajibu wa kutoa taarifa kwa umma kwa wawekezaji waliopo na watarajiwa.

Muundo wa Utawala bora wa Kampuni unajumuisha kusimamia na kudhibiti mahusiano kwa wadau wote kama vile wanahisa, wajumbe wa Bodi, wafanyakazi, wateja, wazabuni na jamii kwa ujumla. kwa ziada, utawala bora wa kampuni ni pamoja na kujituma kufuata misingi na maadili ya kazi, inayotoa muongozo katika biashara na mahusiano ya wadau.

KWA IDHINI YA BODI

Imesainiwa

Tarehe

other material information for a period of three weeks. Risk and compliance Department is responsible for monitoring to ensure that there are no breaches to this Policy.

Compensation of Key Management Personnel

Key Management of the bank is comprised of the Managing Director, Deputy Managing Directors, Director of Internal Audit and all Directors reporting to the Managing Director and Deputy Managing Directors. The remuneration of key management personnel during the year was TZS 5,145 million (2012: TZS 4,592 million).

Related Party Transactions

Parties are considered to be related if one party has the ability to control the other party or exercise significant influence over the other party in making financial or operational decisions. In the normal course of business, a number of banking relationships are entered into with related parties' i.e. key management staff, Directors, their associates and companies associated with Directors. Such relationships are guided by Policies approved by the Board to ensure the same are done at arm's length.

Loans and advances to companies associated with Directors amounted to TZS 8 million (2012: TZS 68 million), while loans and advances to Directors and other key management personnel amounted to TZS 4.2 billion (2012: TZS 3.86 billion). The volumes of related party transactions for the year and the outstanding amounts at the year-end are provided under note 39 of the financial statements.

Ethical Behaviour and Organization Integrity

The Group's corporate governance structure involves managing and controlling relations shared amongst different stakeholders including shareholders, Board of Directors, employees, customers, suppliers and the community at large. Additionally, the corporate governance is also about commitment to values and ethical business practices as enshrined in the CRDB Code of Ethical conduct, which governs all its business interactions and relationships to stakeholders.

BY ORDER OF THE BOARD

Signed

Date



Benki ya CRDB, inatambua kwamba mahusiano ya muda mrefu ndani ya kundi yanahitaji mtazamo wa pamoja na kuwianisha kati ya utendaji wa huduma za kifedha na zile zisizo za kifedha ndani ya kundi. Kwa hiyo basi, ripoti hii, inalengo la kuainisha masuala muhimu yahasikanayo na mahusiano endelevu kwa wadau wetu. Ili kukuza biashara za kundi, tunaendelea kutathimini mazingira yetu ya biashara ili kubaini, ni masuala gani yanaathari kwa mazingira hata kuwa na matokeo chanya kwa wadau wetu.

Benki ya CRDB, inakubali kwamba tunafanya biashara katika mazingira, ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kisheria na kimamlaka, sababu ambazo zinaweza kuwa na athari kwa uendeshaji biashara wa kundi kwa siku za baadaye. Familia kubwa ya wadau, inajumuisha wanahisa wa Benki ya CRDB, wateja wetu, wafanyakazi, watoa huduma, mamlaka za udhibiti, taasisi na idara za serikali pamoja na jamii pana zaidi. Jitahada zetu za kuendeleza uhusiano zimelenga katika kuwianisha mkakati wa Benki na mwendelezo wa kuboresha uhusiano na wadau wetu.

MAJUKUMU YA KIJAMII

Mfumo wa uendeshaji biashara wa Benki ya CRDB, umejikita katika sera ya uwekezaji kwa jamii, ambayo inaelekeza Benki ijihusishe na kujishughulisha na shughuli za kijamii hata ionekane ni raia mwema mbele ya jamii ya Tanzania na Burundi. Benki inaamini katika kuendeleza mahusiano mazuri ya kijamii.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1996, Benki imekuwa ikitoa misaada ya kifedha na isiyo ya kifedha katika maeneo tofauti tofauti ya kijamii, ili kuwezesha jamii kupata mafanikio makubwa. Kila mwaka Benki hutoa misaada mbalimbali kwa jamii stahiki ili kusaidia kufanikisha malengo ambayo jamii imejiwekea katika kuboresha maisha ya watu wake. Mwaka 2013, Benki imechangia kwa mafanikio maendeleo ya jamii katika sekta za afya, elimu na utunzaji wa mazingira.

Kwa mujibu wa sera elekezi, Benki hutumia nguvu kazi ya wafanyakazi katika kufanikisha mchakato wa kusaidia maendeleo ya jamii katika elimu, afya na utunzaji wa mazingira. Benki ya CRDB, inaamini kwamba kupitia elimu hali ya maisha ya wananchi

CRDB Bank PLC recognises that the long term sustainability of the Group requires a joint focus and balance between financial and non-financial performance measures of the Group. This report therefore aims to outline the sustainability issues relevant to the Bank's stakeholders. In order to sustain the business growth of the Group, we continuously scan our environment to identify issues that shape our environment and that can impact positively all our stakeholders.

CRDB Bank PLC accepts that we operate in an environment where social, economic, political, environmental, legal and regulatory factors impact on the future performance of the Group. Our wider stakeholder family includes CRDB Bank PLC shareholders, our esteemed customers, employees, suppliers, regulators, government agencies and departments and the wider public. Our continuous sustainability efforts are directed at aligning the group's strategy to the continuous improvement of our relationship with our stakeholders.

CORPORATE SOCIAL RESPONSIBILITY

CRDB Bank PLC's business model is anchored on a robust Corporate Social Investment (CSI) policy that guides the Bank's involvement in community initiatives as a corporate citizen in Tanzania and Burundi. The Bank believes in playing an active role in promoting sustainability and social consciousness.

Since its establishment in 1996, CRDB Bank has continuously provided financial and non-financial support to a range of sustainable causes with the view of enabling the respective causes to achieve optimal impact. Every year, CRDB Bank makes donations and/or grants to deserving community initiatives and causes that demonstrate a direct impact on the lives of the people within the respective communities. Over the course of 2013, the Group has been actively involved in many positive causes that gave back to the communities in which it operates. The Group has successfully contributed to, as well as participated in, a number of causes focusing on health, education and the environment.

itaboreka na taifa litastawi kwa kuwa na watu wenye afya njema. Lakini haya yote yanawezekana kutekelezeka katika mazingira yenye mahusiano mazuri, na hili linawezekana kwa kuwajibika pamoja.

AFYA

Katika mwaka 2013, jitihada za Benki kwa upande wa majukumu ya kijamii zilijikita zaidi katika kuchangia uboreshaji wa huduma za afya ya jamii, hususani afya ya mama na mtoto. Benki ilijenga na kukarabati wadi za akina mama na watoto katika hospitali kubwa za rufaa katika mikoa mitatu hapa nchini. Hospitali zilizofaidika na mpango huu ni hospitali ya mkoa wa Morogoro, hospitali ya rufaa meta mkoa wa Mbeya na hospitali ya rufaa ya Bugando mkoa wa Mwanza. Mbali na kukarabatiwa, pia hospitali zote tatu zilikabidhiwa na Benki vifaa mbalimbali vya hospitali yakiwemo mablanket, mashuka, magodoro, vyandarua na nk. Jumla ya shilingi milioni 250 zilitumika katika kufanikisha haya yote.

Pia Benki ilitoa mchango kwa taasisi ya St. Laurent inayojihusisha na kampeni dhidi ya ugonjwa wa kisukari. Mchango ulilenga kufanikisha kampeni ya wiki nzima kuhamasisha umma kuhusu ugonjwa wa kisukari. Pia Benki ilichangia kampeni za AMREF zilizojulikana kama “Simama kwa ajili ya mama wa Afrika”

Mwaka 2013, umeingia katika historia ya Benki ya CRDB kama mwaka wa “Mama na Mtoto”. Katika kipindi chote cha mwaka wa fedha, 2013, Benki ilitoa mchango mkubwa katika kuboresha afya ya mama na mtoto kwa ajili ya ukarabati wa wadi za akina mama na watoto katika hospitali kuu za rufaa katika Tanzania.

Uamuzi wa Benki kuwekeza katika ukarabati wa wadi za akina mama na watoto ulitokana na hitaji kubwa la jamii katika kupunguza ongezeko kubwa la vifo vya watoto wachanga na pia haja ya kuboresha mazingira ya afya kwa akina mama waja wazito. Pia kusudi la Benki katika kuhifadhi kizazi kijacho lilichochea Benki kuwekeza katika eneo hili. Benki ya CRDB, inaamini kwamba ustawi wa Tanzania umo katika mikono ya kizazi cha sasa na kijacho, na kupitia kina mama pekee kizazi hiki kinaweza kuhifadhiwa na kuendelezwa.

UKARABATI WA WADI YA AKINA MAMA NA WATOTO

Mpaka kufika mwisho wa mwaka wa fedha 2013, Benki ya CRDB, ilitumia jumla ya shilingi milioni 250 katika ukarabati wa wadi za akina mama na watoto katika

As a matter of policy, the bank utilizes the collective strengths of its workforce to support the community in areas of Education, Health and Environment. CRDB Bank PLC believes that through education, living standards will continuously improve while a healthy nation will prosper. But all these can only be achieved in a sustainable environment, which is a product of collective responsibility.

HEALTH

In 2013, the Banks main CSR efforts were centred in improving healthcare services, particularly to mother and child. The Bank constructed and refurbished maternity and children’s wards in major hospitals in three major regions in the country. The hospitals that benefited were Morogoro Regional Hospital, Meta Referral Hospital in Mbeya and Bugando Referral Hospital in Mwanza. Apart from renovation of the wards, the three hospitals were also furnished with hospital beds, mattresses, bed sheets, blankets and other medical equipment. A total of 250 million was spent on these causes.

The Bank also donated to St. Laurent Diabetes Centre to facilitate a month long diabetes awareness campaign and AMREF Tanzania in facilitating a special awareness campaign dubbed “Stand up for African Mothers”.

The year 2013 goes down in the history of CRDB Bank as “the year of the mother and child”. Throughout the FY, CRDB Bank contributed immensely towards improving the health of mothers and children through targeted donations and grants that were largely channelled towards renovation or maternity and children wards in major referral hospitals across Tanzania.

The Bank’s decision to invest in mother - and - child health was informed by the rising need to improve maternity care and reduce infant mortality rate in Tanzania. Also, the overarching desire to preserve the future generations played a significant role in identifying this project. CRDB Bank believes that Tanzania’s prosperity rests in the hands of the current and future generation and mothers are the only way that these generations can be perpetuated.

MATERNITY AND CHILDREN’S WARD RENOVATIONS

By end of the financial year 2013, CRDB Bank had spent a total of TZS250 Million towards renovations of Maternity and Children wards in three regional referral Hospitals in Tanzania - Morogoro Regional Hospital, Meta Referral Hospital in Mbeya and Bugando Referral

hospitali za rufaa katika mikoa mitatu ya Tanzania, ambazo ni hospitali ya mkoa Morogoro, hospitali ya rufaa Meta Mbeya na hospitali ya rufaa Bugando Mkoa wa Mwanza. Ukarabati wa hospitali hizi ulijumuisha kufumua na kujenga upya mifumo yote iliyoharibika, kama mfumo wa mabomba ya maji safi na taka na pia kuweka vifaa vifya vya hospitali. Vifaa vipya ni pamoja na mablanketi, mashuka, magodoro, vitanda, vyandarua kwa ajiri ya kudhibiti ugonjwa wa malaria nk.

Ili kufanikisha, mchakato huu, Benki hutumia hazina kubwa ya wafanyakazi wake wenye ujuzi katika fani mbalimbali mfano katika usanifu wa majengo, unesi nk ili kupunguza gharama itokano na kukodi wataalam wa nje ambao kimsingi wanagharama kubwa. Kwa namna hii hamasa ya ushiriki wafanyakazi iliongezeka kwa kiasi kikubwa ndani ya Benki.

KUAHAMASISHA KUHUSU UGONJWA WA KISUKARI

Ugonjwa wa kisukari, umeendelea kuwa tatizo kubwa katika dunia. Aina ya 1 na ya 2 ya kisukari imeendelea kuuwa watu wengi zaidi duniani. Kwa umuhimu Benki inaweka kwa afya ya binadamu, pale taasisi ya St. Laurent inayohusika na ugonjwa wa Kisukari ilipoleta ombi la kuitaka Benki ichangie katika kampeni za uhamasishaji dhidi ya ugonjwa huu, Benki haikusita bali ilikuwa mstari wa mbele katika kampeni za kudhibiti vifo vitokanavyo na ugonjwa wa kisukari. Pia Benki ilichangia kampeni kupitia shirika la AMREF, iliyoitwa “*Simama kwa ajili ya mama wa Afrika*”

UKIMWI

Ugonjwa wa UKIMWI umendelea kuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya Bara la Afrika. Tanzania haiko nje ya tatizo hili. Benki ya CRDB, inatambua uwepo wa Tatizo hili. Mbali na kuhimiza watu kuishi kwa kuwajibika, Benki imechukua hatua za makusudi kupunguza madhara yatokanayo na UKIMWI. Katika mwaka wa fedha wa 2013, Benki ilichangia shilingi milioni 30 kwa mfuko wa Benjamini Mkapa Foundation unaojijhusisha na kampeni mbalimbali dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

ELIMU

Katika mwaka 2013 Benki iliendelea na jitihada zake za kuchangia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mpango mkakati wake wa kujitana. Pia Benki ilichangia Chuo Kikuu cha St. John kilichopo Dodoma. Benki pia ilichangia Shule ya msingi Toa-Ngoma iliyopo Dar es Salaam ili kusaidia shindano la kitaaluma sanjari na ujenzi wa vyumba vya madarasa



Hospital in Mwanza. The refurbishments and renovations comprised complete overhaul of dilapidated facilities, fresh plumb works and furnishing. Furnishing included acquisition of a range of hospital facilities such as beds and beddings, mosquito nets (to mitigate the spread of malaria) and other medical equipment.

To maximize the impact of donations, CRDB Bank repeatedly tapped into the expertise of its employee base for specialized skills such as architects, nurses and other professionals among its workforce to volunteer their skills and manage the projects to reduce costs of hiring external professionals who are at times very expensive. The exercise was met with excitement and satisfaction that largely boosted the employee morale across the bank.

DIABETES AWARENESS

Diabetes remains a major health problem globally. Type 1 and 2 strains of Diabetes are among the top killer diseases around the world. With the importance that CRDB Bank attaches to human life, the CSR team - when approached by St. Laurent Diabetes Centre actively took part in creating awareness about the disease with the aim of mitigating related deaths. The Bank facilitated the month - long campaign dubbed “Stand Up for African Mothers” in conjunction with AMREF Tanzania

HIV/AIDS

The AIDS pandemic in Africa still remains a crippling factor to the economic well-being many countries. Tanzania is not an exception. CRDB Bank is conscious of this problem and besides advocating for responsible living, the Bank has also deliberately contributed towards mitigating the effects of HIV/AIDS. In the FY 2013, CRDB Bank made contributions totalling to TZS 30 Million to the Benjamin Mkapa Foundation which complements government efforts in enhancing the delivery of quality HIV and AIDS care, treatment and other related services including Reproductive and Child Health to Tanzanians.

Kwa kuzingatia sera ya kuwekeza katika jamii, misaada kwa sekta ya elimu imeendelea kuwa mikubwa zaidi kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Benki ya CRDB ilijikita katika kufadhili miradi mbali mbali ya shule, lengo na madhumuni likiwa kukijengea uwezo wa kimaarifa kizazi kijacho. Jumla ya shilingi milioni 29 (takribani 7% ya bajeti ya mwaka 2013 kuhusu majukumu ya Benki kwa jamii) ilitumika katika elimu na utafiti kuhusiana na miradi ya elimu.

Benki ya CRDB, imekuwa mdau muhimu kwa Chuo kikuu cha Dar es Salaam katika mpango mkakati wake wa kujipanua hususani katika uanzishwaji wa kitivo kipya cha elimu. Benki ilichangia shilingi milioni 100 katika mwaka wa fedha 2012 na Benki imepanga kuchangia tena shilingi milioni 50 katika mwaka wa fedha 2014 kwa ajili ya upanuzi wa chuo.

Hali kadhalika, katika mwaka wa fedha 2013, Benki ilitoa pia michango mbalimbali katika miradi mbali mbali ya elimu, kama katika chuo kikuu cha St John kilichopo mkoani Dodoma. Pia Benki ilitoa udhamini mbalimbali katika sekta ya elimu ya shule ya msingi, mfano katika shule ya msingi Toa-Ngoma, iliyopo Dar es Salaam, ambapo Benki ilitumia shilingi milioni 5 kununua vitabu na madawati kwa ajili ya wanafunzi. Pia Benki ilishirikiana na mamlaka ya elimu Tanzania, katika kampeni za ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika shule zilizokuwa zimechaguliwa.

EDUCATION

In the year 2013, the Bank continued with its support to the University of Dar es Salaam in facilitating its expansion strategy. The Bank also donated to St. John University in Dodoma and Toa-Ngoma primary school in Dar es Salaam to support student's academic competition and construction of classrooms respectively.

Pursuant to the CRDB Bank Corporate Social Investment Policy, support to education causes and initiatives remains paramount every year. In the Financial year 2012/2013, the Bank continued its commitment to supporting education projects with the view of empowering the young generation through knowledge. A total of TZS29 million (about 7% of the 2013 CSR budget) was spent on education and research related projects within the FY, in addition to already existing projects within the sector.

Elsewhere, CRDB Bank is a key partner in the University of Dar Es Salaam expansion program in which the university is developing a new faculty (Education). The Bank has contributed up to TZS100 Million since 2012 and is set to contribute an additional TZS50 million in the 2014 Financial Year towards the expansion.

Similarly, the bank during the financial year made contributions to various projects at St John's University in form of sponsorships besides undertaking other projects in primary schools such as Toa- Ngoma Primary in Dar es Salaam where the Bank contributed over TZS5





Katika, sekta ya utafiti, Benki ya CRDB, imeendelea kujitoa katika kufadhili tafiti mbalimbali, ili kuchochea ugunduzi mbalimbali katika nyanja za kijamii na kiuchumi. Katika mwaka wa fedha 2013, Benki iliendelea kudhamini tafiti mbali mbali kupitia taasisi ya utafiti wa masuala ya kijamii na kiuchumi (ESRF). Benki ilichangia jumla ya shilingi milioni 5.

MAZINGIRA

Benki ya CRDB, imeendelea kujituma zaidi katika utunzaji wa mazingira, kwa kuhifadhi rasilimali chache zilizo, kwa njia ya ufanyaji biashara kwa kuzingatia uoto wa kijani. Benki imekuwa ikiwahamasisha wateja wake na jamii kwa ujumla kushiriki katika uhifadhi wa mazingira. Benki ya CRDB, imekuwa mstari wa mbele na kinara katika kuchangia shughuli mbalimbali za uhifadhi wa mazingira, ikianza na uanzishaji wa huduma ya kutoa taarifa ya mwezi ya akaunti ya mteja kwa njia ya mtandao pasipo kutumia karatasi. Huduma hii inajulikana kama “ e-statement”. Ni njia ya kieletroniki ya kumtumia mteja taarifa yake ya mwezi ya akaunti kupitia barua pepe yake.

Pia Benki imekuwa inatoa msisitizo, ili wateja watumie zaidi huduma za kibenki kupitia simu za mkononi na mtandao wa intaneti, kwani huduma hizi, hazihitaji matumizi ya karatasi. Ubunifu huu jadidi, umesaidia kupunguza kiasi kikubwa cha karatasi ambacho

Million towards the purchase of books and desks for pupils. Also working with the Tanzania Education Authority, the bank contributed TZS10 million towards construction or boarding facilities for girls in selected schools.

In Research, CRDB Bank remains committal to the sponsorship of various research studies to foster social and economic innovation. In the FY 2013, the bank continued with its sponsorship to the Economic and Social Research Foundation Funds (ESRF) to the tune of TZS5 Million among other forms of support.

ENVIRONMENT

CRDB is committed to a “greener” way of doing business by continually conserving the limited natural resources and helping its customers and communities do the same. In so doing, the Bank has been a champion of supporting environmental conservation activities starting with introduction “paper-less” way of sending monthly statements to customers named “e-statement”. This is an electronic way of sending monthly statement to our customers via emails. The Bank also emphasised on usage of SimBanking and electronic banking services that are cell phone and internet based services requiring no paper work. These innovations have significantly reduced the amount of paper that was previously used for the objectives.

kimekuwa kinatumika. Kwa kutumia teknolojia hizi za kutoa huduma za kibenki kwa wateja kwa njia ya simu za mkononi na kwa mtandao wa intaneti Benki imefanikiwa kupunguza matumizi ya karatasi kwa 70% katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita.

Benki ya CRDB, imejitoa kwa dhati katika kutunza uoto wa kijani ili kuwa na mazingira mazuri yaliyo endelevu. Kwa kutumia mipango mbalimbali ambayo Benki imejiwekea ndani na nje ya Benki, lengo ni kupunguza madhara yatokanayo na gesi ya kaboni na kujikita zaidi katika uboreshaji wa mazingira.

Katika kuimarisha utamaduni wa wafanyakazi wake kupenda kutunza mazingira, Benki huwashirikisha wafanyakazi wake moja kwa moja katika zoezi la upandaji miti. Wakati wa ukarabati wa wodi za akina mama waja wazito na watoto katika hospitali kuu za rufaa zilizo mikoa mitatu kama zilivyoainishwa hapo awali, wafanyakazi wa Benki kwa ujumla walipanda miti 10,000 na miche ya maua ipatayo 2,000, ili kuboresha mazingira ya hospitali.

Kwa upande mwingine, Benki pia imekuwa inajihusisha na ufadhili wa tafiti mbalimbali zinazohusu uhifadhi wa mazingira, hususani kupitia taasisi ya upembuzi wa rasilimali (IRA) na taasisi inayojihusisha na utafiti wa masuala ya kiuchumi na kijamii. Pia Benki ya CRDB, ilichangia mradi wa maji katika kijiji cha Kilemela, wilaya ya Bagamoyo, katika mkoa wa Pwani. Benki inaamini kuwa, tafiti kama hizi, zinaweza saidia kupata suluhisho kwa matatizo mbalimbali yanayochochea uharibifu wa mazingira.

Utekelezaji wa mipango yote ya Benki inayohusu uwekezaji katika jamii, unaongozwa na sera husika, ambayo inasimamiwa kwa dhati kabisa kwa kufuata vigezo vilivyopitishwa na si vinginevyo. Kwa msingi huu, maombi yanayo pokelewa na kukubaliwa ni yale tu yaliyokidhi vigezo kwa misingi ya utekelezaji wa wazi, ili kuifanya dunia kuwa mahali bora pa kuishi.

CRDB bank is committed to adopting green solutions for environmental sustainability. Through various initiatives both within and without the bank, CRDB Bank is focused on reducing the carbon footprint and significantly contributes towards the improvement of the environment.

Among the initiatives adopted within the business towards environmental sustainability include transition from paper-based to paperless banking, which kicked off with the issuance of e-statements that is aimed at reducing the use of paper. Under this initiative, CRDB bank customers receive their monthly statements electronically as opposed to hard copy as previously done. Similarly, the bank has adopted and integrated modern technologies such as Simbanking and Internet Banking to reduce reliance on paperwork. Adoption of these banking technologies has reduced the use of paper by up to 70 % over the past couple of years.

To further promote environmental consciousness, CRDB Bank has made it a tradition to involve its staff members in tree planting exercises. During the renovations of the maternity and children wards in the three provinces listed above, CRDB Bank staff collectively planted up to 10,000 tree seedlings and 2,000 flower seedlings at the hospitals to improve the environment.

On the other hand, the bank has been active in sponsoring environment related research carried out by the Institute of Resource Assessments (IRA) and the Economic and Social Research Foundation Funds (ESRF). The Bank also supported water projects in Kilemela Village in Bagamoyo, Pwani. CRDB strongly believes that studies like these will bring solutions to various challenges that prompt environmental degradation activities.

The CRDB Bank social investment initiatives are based on merit and strictly adhere to the provisions of the Bank policies. The bank remains receptive to justifiable proposals and transparent engagements that are aimed at making the world a better place.

Bodi ya wakurugenzi inao wajibu wa kuanzisha na kusimamia mfumo wote wa kusimamia viashiria vyote vya hatari kuhusu Kundi. Kama sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wake kuhusu utawala bora, Bodi ya wakurugenzi imetengeneza mfumo wa kusimamia viashiria vya hatari kwa kuvibainisha, kuvipima na kuvidhibiti (kwa kuweka vigezo vya kudhibiti) na kuvisimamia viashiria vya hatari za Kundi. Sera zote kuhusiana na viashiria vya hatari zimejumuishwa katika mfumo mkuu wa Benki unaodhibiti taarifa mbalimbali za Kundi, pia sera za benki zinathibitishwa na kudhibitiwa na mfumo thabiti wa utoaji taarifa.

Bodi ya wakurugenzi, inawajibika kwa kila suala kuhusu viashiria vya hatari na pia inahusika na udhibiti wa ndani wa viashiria vyote vya hatari. Bodi ya wakurugenzi imekasimisha jukumu lake la kudhibiti viashiria vya hatari kwa uongozi wa juu wa Benki kwa kuchagua kamati ndogo ambazo ni kamati ya viashiria vya hatari, ya ukaguzi wa mahesabu, ya utawala bora na rasilimali watu na ile ya mikopo katika kiwango cha Bodi. Uongozi wa juu wa Benki husimamia udhibiti wa viashiria vya hatari vya Benki kupitia kamati ya usimamizi wa viashiria vya hatari ambayo ni mwangalizi mkuu wa mfumo wote wa Benki kuhusiana na wigo wote wa viashiria vya hatari, ilhali kamati ya rasilimali na madeni (ALCO) inahusika na usimamizi/udhibiti wa viashiria vya hatari za kifedha ambazo zinaweza kuwa na athari katika miazania ya Benki. Kamati hizi zote kuhusu usimamizi wa viashiria vya hatari hukutana mara moja kila mwezi ili kutathimini kiwango cha viashiria vya hatari dhidi ya malengo ambayo Benki imejiwekea. Kamati zote mbili hutoa taarifa kwa Bodi ya wakurugenzi katika kila robo ya mwaka.

Hata hivyo, ni wajibu wa kila mfanyakazi kutoa ushirikiano katika kudhibiti viashiria vya hatari, kupitia shughuli zake za kila siku. Msingi wa kufanikisha mchakato huu ni kuwa na mawasiliano yanayozingatia malengo na madhumuni ya Bodi. Ikizingatiwa kwamba. Bodi imeweka mfumo jumla wa kusimamia na kudhibiti viashiria vya hatari, sanjari na uwepo wa sera na taratibu za kuwaongoza wafanyakazi. Sera zinaweka wazi kiwango cha juu kabisa cha viashiria vya hatari na viashiria vya taarifa kwamba sasa Benki inaweza

The Board of Directors has overall responsibility for the establishment and oversight of the Group's risk management framework. As part of its governance structure, the Board of Directors has embedded a comprehensive risk management framework for identifying, measuring, controlling (setting risk mitigations) and monitoring of the Group's risks. The policies are integrated in the overall management information systems of the group and supplemented by a management reporting structure.

The Board of Directors accepts ultimate responsibility for the risk management and internal control function of the Bank and has delegated the process to senior management through its sub-committees which are the Risk, Audit, Governance and Human Resources and Credit committees at the Board level. The senior management in turn oversees risk management through the risk management committee which is in charge of the entire scope of risks and the ALCO committee that is in charge of financial risks impacting the balance sheet. Both these management committees meet monthly to review the Bank's risk profile and performance vs. set targets. The two committees report quarterly to the Board risk committee.

However it is the responsibility of every employee to support the process by managing risks inherent in their day to day operations. Key to this process is communication of the Board's objectives and the Board has in place the Group Risk Management framework and Risk Management Policies and procedures to guide staff. The policies clearly set out risk limits and triggers to alert the Bank of potential losses from undertaken risks for timely remedial action. The senior management ensures that adequate internal control systems are developed and maintained on an ongoing basis in order to provide reasonable assurance regarding all aspects related to risk management in the Bank.

Efficiency of any governance process is dependent on the strict observance of prescribed measures and in order to ensure the controls remain adequate, the Bank has established a fully-fledged and independent risk and compliance function. The risk and compliance department coordinates and oversees the

kupata hasara, ili Benki iweze kuchukua hatua za tahadhari. Uongozi wa juu wa Benki unahakikisha kwamba mfumo wa udhibiti wa ndani wa viashiria vyote vya hatari unaendelea kuwa thabiti na endelevu ili kuwa na hakika ya kwamba hatari zote ndani ya Benki zimedhibitiwa.

Ufanisi katika taratibu za utawala bora unategemea sana uzingatiaji wa taratibu zote za kutathimini na kudhibiti viashiria vya hatari, kwa msingi huu Benki, imeanzisha kitengo mahususi cha kusimamia uzingatiaji wa taratibu zote zinazohusika na udhibiti wa viashiria vya hatari. Idara ya usimamizi wa viashiria vya hatari na uzingatiaji wa taratibu, inahusika na uratibu wa utekelezaji wa taratibu zote zihusikanazo na udhibiti wa viashiria vya hatari ndani ya Benki, idara hii hutoa taarifa zake kwa mkurugenzi mtendaji wa Benki. Pia, wakaguzi wa ndani wa mahesabu ya Benki, hukikagua na kukitathmini kitengo cha usimamizi wa viashiria vya hatari sanjari na uzingatiaji wa taratibu husika za kudhibiti viashiria vya hatari, na kisha kutoa ripoti kwa kamati ya Bodi inayohusika na ukaguzi wa mahesabu. Wakaguzi wa nje na mamlaka ya udhibiti, hutoa taarifa kwa mkurugenzi mtendaji na kwa Bodi kuhusiana na uendeshaji wa mfumo wa ndani wa udhibiti ambao umefanyiwa tathmini kama sehemu ya utaratibu wa kila mwaka wa ukaguzi na tathmini ya mamlaka ya udhibiti.

Tathmini ya Sera

Benki ya CRDB, kwa kuzingatia kuwa ni Benki inayo ongoza katika soko, inachukulia kwa umakini sana suala zima la usimamizi wa na udhibiti wa viashiria vya hatari katika shughuli zake za kila siku. Benki inawajibika kwa wanahisa wake na kwa jamii yote kwa ujumla kulinda rasilimali, amana na mtaji huku ikichangia kukua kwa uchumi wa nchi.

Katika mwaka wa fedha 2013, Bodi ilifanya tathmini sera zote na kiwango cha juu kabisa kihusikanacho na shughuli za Benki. Mapitio mapya ya sera ya udhibiti wa viashiria vya hatari ndani ya Kampuni yalizingatia uanzishwaji wa kampuni tanzu ya Benki ya CRDB nchini Burundi, ili kufanikisha wa utekelezaji wa mpango mkakati wa utawala bora. Bodi ilianzisha rasmi sera ya kudhibiti na kusimamia hatari zitokanazo na udanganyifu.

Mpango wa usimamizi wa viashiria vya hatari

Shughuli za kampuni zinaathiriwa kwa namna nyingi na viashiria vya hatari za kifedha, na viashiria hivi vinahitaji upembuzi, tathmini na kukubalika kwa

implementation of the enterprise wide risk management framework within the Bank, reporting directly to the Managing Director. Additionally the Bank's internal auditors review the risk management function and report directly to the Board's audit committee. External auditors and the regulator provide feedback to the Managing Director and the Board on the operation of the internal controls reviewed as part of the annual audit and regulatory review respectively.

Policy Reviews

CRDB Bank by virtue of its position as a leading Bank considers Risk Management vital in its daily business. The Bank has a responsibility to the public and shareholders to safeguard assets, deposits and capital held with it while also upholding contribution to the country's economic growth.

During the year under review the Board reviewed all policies and authority limits governing operations of the Bank. Fundamental review was done in respect of the Group Risk Management Framework to accommodate governance in relation to the Burundi subsidiary. The Board introduced a new policy for Fraud Risk Management.

Risk Management Framework

The Group's activities expose it to a variety of financial risks and those activities involve the analysis, evaluation, acceptance and management of some degree of risk or combination of risks. Taking risk is core to the financial business, and the operational risks are an inevitable consequence of being in business.

The Group's aim is therefore to achieve an appropriate balance between risk and return and minimize potential adverse effects on the Group's financial performance. The Group's risk management policies are designed to identify and analyse these risks, to set appropriate risk limits and controls, and to monitor the risks and adherence to limits by means of reliable and up-to-date information systems. The group regularly reviews its risk management policies and systems to reflect changes in markets, products and emerging best practice.

Financial risks

Financial risks include credit, liquidity and market risks. The Bank's overall risk management policies are set out by the Board and implemented by the Management. These policies involve identification, evaluation, mitigation and monitoring of such risks. The most

uongozi wa Benki kwa kiasi fulani cha viashiria vya hatari au mseto wa viashiria vya hatari. Kukubali kiwango fulani cha viashiria hatari ni jambo ambalo haliepukiki katika biashara ya fedha, na hatari zitokanazo na uendeshaji wa biashara hii ni madhara ambayo yanatokana na kuwa katika biashara hii.

Madhumuni ya kampuni ni kufanikisha uwiano mzuri kati ya madhara yatokanayo na hatari za kibiashara dhidi ya mafao ya kibiashara, huku madhara mabaya kwa biashara ya fedha yakipunguzwa kwa kiasi kikubwa. Sera ya kampuni kuhusu udhibiti wa viashiria vya hatari imetengenezwa kwa namna ambayo inaruhusu kuainisha na kupambanua viashiria vya hatari, na kisha kuweka ukomo wa viashiria hatari na mikakati muafaka ya udhibiti sanjari na uzingatiaji wa taratibu za ukomo kwa kutumia mfumo wa kisasa wa habari. Kampuni hufanya mapitio ya mara kwa mara ya sera zake kuhusu usimamizi wa udhibiti wa viashiria vya hatari na mifumo yake yote ili kwenda sambamba na mabadiliko katika soko, katika bidhaa na katika kanuni za utendaji makini.

Viashiria vya hatari za kifedha

Viashiria vya hatari za kifedha vinajumuisha vile katika mikopo, uwingi au uhaba wa fedha na viashiria hatari katika soko. Sera zote zinazohusika na usimamizi wa viashiria vya hatari katika biashara za Benki zinapangwa na Bodi na kutekelezwa na uongozi wa Benki. Sera hizi zinahusisha ubainishaji wake, utathmini wake, udhibiti wake na usimamizi wake. Katika kundi hili, viashiria vya hatari ni:

- Viashiria vya hatari za mikopo
- Viashiria vya hatari za hali ya fedha
- Viashiria vya hatari za soko (kiwango cha riba, biashara ya fedha za kigeni na hatari za bei)

Viashiria vya hatari za Mikopo

Kundi na Benki vinakumbana na viashiria vya hatari kupitia mikopo, ambapo mshirika wa biashara anashindwa kutimiza wajibu wake. Viashiria vya hatari kupitia mikopo ni vya muhimu zaidi kuangaliwa katika biashara ya Kundi, uongozi wa Benki unapaswa kudhibiti kwa makini sana viashiria vyote vya hatari kupitia mikopo. Viashiria vya hatari kupitia mikopo, hutokea sana kupitia

Shughuli za ukopeshaji, kupitia dhamana za mikopo na kupitia gharama mbalimbali za rasilimali za Benki. Pia kuna viashiria vya hatari kupitia shughuli nje ya mfumo wa mizania ya Benki kama vile dhamira ya ukopesha, udhamini katika biashara ya nje na garantii. Mfumo wa usimamizi na udhibiti wa viashiria vya hatari kupitia

important type of risks in this group are:

- Credit risk
- Liquidity risk
- Market risk (interest rate, foreign exchange and price risks)

Credit risk

